# Ushujaa katika Motifu ya Safari ya Msako na Utamaduni na Falsafa ya Kiafrika

Felix K. Sosoo
Chuo Kikuu cha Ghana

**Ikisiri**

Utamaduni ni mfumo wa maisha au jinsi watu wanavyoishi katika jamii fulani. Mfumo huu unaundwa na vipengele mbalimbali kama vile mavazi, lugha, sanaa za maonyesho, imani, mila desturi, na kadhalika. Lengo la makala hii ni kuchunguza namna ushujaa katika motifu ya safari ya msako unavyoakisi utamaduni na falsafa ya Kiafrika ukilinganishwa na mtazamo na maoni ya wataalamu na watafiti mbalimbali kuhusu falsafa ya Kiafrika. Swali linaloulizwa na wengi ni: je, ni kweli kuna falsafa ya Kiafrika? Kwa vile lengo katika makala hii ni kuchambua utamaduni na falsafa ya Kiafrika vinazojitokeza katika ngano za Kiewe na riwaya teule za Shaaban Robert, ni vizuri kwanza kuthibitisha kama kuna falsafa ya Kiafrika katika riwaya teule na ngano za Kiewe. Vipengele vya ontolojia vilivyoshughulikiwa katika makala hii ni: uzazi, umoja na mshikamano, uchawi na uganga (sihiri), na imani katika kifo na roho (maisha baada ya kifo). Vipengele hivi vya falsafa ya Kiafrika vimechambuliwa kuonesha namna vinavyosawiriwa katika ngano teule za Kiewe na riwaya moja ya Shaaban Robert ambayo ni *Kufikirika.*

## 1.0 Utangulizi

Kuna wataalamu mbalimbali waliozungumzia aina mbalimbali za safari ya shujaa. Kwa mfano, Kunene (1985) ameangalia safari ya shujaa kwa namna mbili; safari ya nje na ya ndani au kisaikolojia. Safari ya nje inahusisha mwendo wa kutoka sehemu moja hadi nyingine wakati safari ya ndani ni masafa mafupi. Naye Senkoro (1997) aliangalia safari za nje na ndani anaposema kitendo cha shujaa kuondoka mahali alipo na kwenda ugenini huwa ni cha muda mfupi zaidi kuliko ile safari ya ndani ambapo shujaa hupitia hatua za ukuaji kutoka utotoni hadi ukubwani.

Kinachoangaliwa katika makala hii ni safari inayohusishwa na mwendo wa kutoka sehemu moja hadi nyingine ambayo ni ya nje na jinsi ushujaa katika safari ya msako unavyobeba vipengele mbalimbali vya utamaduni na falsafa ya Kiafrika. Vipengele hivyo vinajadiliwa kwa kutumia ruwaza ya shujaa kwa mujibu wa Campbell (1973). Aidha, data zilizotumika katika makala hii ni ya uwandani na maktabani. Data za uwandani zilizokusanywa ni zile zinazohusu motifu ya safari ya

msako katika masimulizi ya ngano za Kiewe. Pia, data zilizopatikana katika riwaya teule ya Shaaban Robert, zilichopolewa wakati wa kuisoma riwaya hiyo. Data za maktabani zilipatikana kwa kusoma na kuchambua machapisho/maandiko yaani vitabu, tasnifu na makala mbalimbali, tovuti na wavuti yanayohusiana na motifu ya safari ya msako.

## 2.0 Ruwaza za Shujaa na Falsafa ya Kiafrika

Kwa mujibu wa ruwaza ya shujaa ya Campbell (1973) shujaa ana hatua tatu. Kwanza ni kuondoka, pili kukutana na vikwazo na kuvishinda, na mwisho ni kurudi katika jamii. Brown (1990) anaunga mkono wazo la Campbell anapobainisha zaidi kwamba hatua ya kwanza ni kuondoka kwa shujaa. Shujaa anasafiri na kwenda nchi za mbali. Hatua ya pili anakutana na vikwazo, misukosuko na majaribu ambayo yanamfunda na kumkomaza. Katika hatua hii shujaa huwa anapata ukomavu wa kififikra na ujasiri zaidi ili aweze kushinda vikwazo hivi. Katika hatua ya tatu shujaa anarejea kwao. Kwa mujibu wa Campbell hiyo ndiyo hatua ya mwisho. Anapofika kwao, shujaa hukaribishwa na kupata hadhi na heshima kubwa na hatimaye kuwa mtawala. Hivyo, katika makala hii ruwaza za Campbell (1973) zilizoibua utamaduni na falsafa ya Kiafrika ndizo zitakazozingatiwa. Nazo ni kuzaliwa kwa shujaa, kuondoka kwa shujaa, shujaa kukutana na majaribu au vikwazo na, kifo cha shujaa. Hata hivyo, kabla ya kufafanua vipengele hivi, tutazungumzia usimulizi wa ngano katika jamii ya Waewe kutoka Ghana pamoja na usuli wake. Aidha, tutatoa usuli wa riwaya teule kisha kufafanua dhana za utamaduni na falsafa ya Kiafrika kama zilivyotumiwa katika makala hii.

## 3.0 Usimulizi wa Ngano katika Jamii ya Waewe

Utanzu wa ngano (ambao kwa Kiewe ni *Gli*) huchukuliwa na Waewe kuwa ni usimulizi wa mdomo unaotumia mbinu za kifasihi za kuwasilisha tamaduni na maisha ya jamii hiyo. Utanzu huu ya fasihi simulizi unatumika kuelimisha jamii ambayo inakuwa katika mfumo wa kuchanganya maadili, mafunzo na burudani kwa pamoja. Maudhui muhimu katika *Gli* ni kukemea tabia mbaya ambayo haikubaliki katika jamii, na kuhimiza tabia njema zinazokubalika katika jamii inayohusika. Halikadhalika, ngano hutumika kuwatia moyo wanajamii katika shida na matatizo mbalimbali. Ngano nyingi hutumia mbinu mbalimbali za kifani katika uwasilishaji wa maudhui yake. Miongoni mwa mbinu maarufu zinazotumiwa ni matumizi ya motifu, na hasa ya safari ya msako. Motifu hii hutumiwa kuwahamasisha wanajamii kujitafutia maisha mazuri kupitia safari ya msako. Aidha, hutumika kuibua maadili mbalimbali muhimu kwa jamii hii.

Akizungumzia kuhusu ngano za Waewe, Dzakpasu (1981) anasema kuwa ngano ni usimulizi wa mdomo, hivyo si rahisi kupata sifa zake za kifasihi mpaka

itendeke na kuchambuliwa kama ilivyosimuliwa kutoka kizazi hadi kizazi. Dzakpasu anaendelea kueleza kuwa ngano ya Kiewe ni fasihi simulizi inayobadilikabadilika na iliyo hai kama tamaduni ambamo inatumika. Vilevile, nguvu ya ngano za Kiewe inaweza kuonekana katika matumizi yake kama mbinu ya kukosoa matendo mabaya katika jamii. Hivyo, Waewe wanatumia ngano kama njia mojawapo ya kuwasilisha na kupitisha falsafa na utamaduni wao kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Katika makala hii, tumeteua ngano maalumu kumi (10) kutoka jamii za Kiewe zinazobeba dhana ya ushujaa katika safari ya msako na kusawiri masuala ya utamaduni na falsafa ya jamii hiyo. Usampulishaji lengwa ndio ulitumika katika uteuzi hizo. Katika zoezi hili, tulikusanya ngano nyingi uwandani, kisha tulizisikiliza na kuchagua zile zinazoendana na mada ya makala hii na tukatafsiri kutoka lugha ya Kiewe hadi Kiswahili.

### 3.1 Muhtasari wa Ngano Teule

Ngano iitwayo "Asiyesikia la mkuu huvunjika guu" inasimuliwa kuwa, hapo zamani za kale, palikuwapo na mashujaa wawili Atsu na Etsey ambao walisafiri pamoja na wazazi wao kwenda shambani na wakasahau filimbi yao shambani. Ushujaa unajidhihirisha kwa Atsu aliposafiri usiku kwenda kutafuta filimbi yao na kuipata licha vikwazo vyote alivyopitia njiani kabla ya kuikuta filimbi yake. Etsey baada ya kupata taarifa za kifo cha kaka yake alifunga safari na kwenda kwa wazee wa kijiji kutoa taarifa. Katika ngano ya "Paka na Panya sio Marafiki", tunasimuliwa kuhusu uadui wa paka na panya ambao walikuwa katika safari ya kutafuta kazi. Baada ya marafiki hawa kupata kazi waliyokuwa wanasaka, waliamua kuoa na kulikuwa na safari nyingine ya kusaka watoto. Katika harakati hiyo, tunaambiwa kwamba paka anamlaumu panya kuwa chanzo cha ugumba wake maana alimpeleka kwa wachawi. Hii ilimfanya paka naye kwenda kwa waganga ili apate suluhu la tazizo lake.

Aidha, ngano iitwayo "Mpewa hapokonyeki" haitofautiani na ile ya "Paka na Panya sio Marafiki". Ngano hii inahusu shujaa mfalme ambaye anadhaniwa kutokamilika kwa sababu ya kutokuwa na mtoto licha ya mafanikio yake. Tatizo hili limemfanya mfalme kuwatafuta waganga na kufanya matambiko ili aweze kupata suluhu kwa ugumba na utasa wake na wa mke wake. Mwishoni, mke wa mfalme anapata mtoto wa kiume ambaye anaonekana kuhatarisha ufalme wa baba yake. Kwa sababu hiyo, mfalme aliamua kumuua mtoto wake ili asikue na kumwondoa kama mfalme kwa mujibu wa watabiri. Baada ya mke wa mfalme kusikia hivyo alitoroka na mtoto ili kutafuta makazi mapya. "Umoja ni Nguvu" ni ngano nyingine inayohusu kisa cha farasi ambaye anatafuta sehemu salama ya kujihifadhi na kuokoa maisha yake baada ya kugundua kuwa mfalme anataka kumwangamiza. Tunasimuliwa kuwa farasi anakutana na mbwa ambaye naye

alitoroka kuuawa. Marafiki hawa wawili pia walikutana na paka na jogoo katika safari yao. Tunasimuliwa namna wote walivyoshirikiana pamoja na kushinda katika safari yao kwa kupata chakula na mahali pa kukaa. Ngano iitwayo "Mkono wa Birika Haufai" inahusu safari ya wanakijiji wakiwa katika harakati ya kujipatia na kumuoa binti mfalme. Buibui katika safari hiyo anaibuka mshindi kwa kumaliza kulima shamba la mfame na kumuoza binti mfalme. Ushujaa unajidhihirisha kupitia mhusika bibi ambaye alifanikisha kuua jini kwa kutumia nguvu ya sihiri kumzidi jini. Aidha, katika ngano ya "Asana na Fuseini" tunasimuliwa kisa cha Fuseini kumezwa na chunusi. Hii imemfanya Asana kuingia katika msako wa kumtafuta kaka yake. Asana analazimika kutumia nguvu ya sihiri aliyopewa na wazazi wake kuzama majini na kupambana na chunusi. Mwishoni anafanikiwa kumuua chunusi na kumuokoa kaka yake na kurudi naye.

Katika ngano iitwayo "Baada ya Dhiki Faraja", msimulizi anatusimulia kuhusu shujaa Kuwornu na mke wake ambao waliishi katika jamii inayothamini sana uzazi. Kuwornu na mke wake walioana na kuwa na furaha tele katika ndoa yao. Aidha, furaha hiyo imegeuzwa kuwa huzuni baada kusafiri sehemu mbalimbali kusaka mtoto miaka mingi bila mafanikio. Baadaye, fanani anatuambia kuwa wamesaidiwa na mganga kupata watoto. Vilevile, katika ngano iitwayo "Ujasiri wa Mmoja Huokoa Taifa", fanani anatuambia namna buibui alivyokuwa anatumia uchawi kuwaua wanyama wengine na kuwala kutokana na balaa la njaa lililoikumba nchi yao. Shujaa Kuchakuro katika ngano hii ameshuhudia mauaji mengi ya wenzake, kwa hiyo, alienda kuweka mkutano na wanyama wengine na wakapata mawazo ya kumteketeza buibui. Wanyama walikuwa na umoja wa hali ya juu na wakamuunga mkono Kuchakuro katika vita dhidi ya buibui, wakafanikiwa kumuua adui na kuwanusuru wanyama wengine. Katika ngano za "Ujasiri wa Mmoja Huokoa Taifa" na "Mkono wa Birika Haufai", tunaoneshwa jinsi uchawi unavyotumika kuharibu na kuua watu wengine. Hadithi hizi zinatuonesha kuwa katika jamii za Waewe, ili uchawi uweze kuwa na madhara kwa anayerogwa, basi mchawi anapaswa kuwa mtu wa karibu sana na yule anayerogwa kama vile rafiki au jamaa.

"Usisahau Asili Yako" ni ngano kuhusu kisa cha mwanamke tasa ambaye alikuwa katika msako wa kumpata mtoto. Mwanamke huyu shujaa anaamua kufunga safari na kwenda mbali msituni kumlilia Mungu ili apate mtoto. Tunasimuliwa pia namna jamii yake inavyomkejeli kwa kukosa mtoto. Katika ngano hii, shujaa anapata suluhu kwa shida yake kwa msaada wa waganga. Kwa upande mwingine, "Pacha na Bibi Kizee" ni ngano ambayo inahusiana na kisa cha Atsu na Etsey. Shujaa Atsu na mwenzake Etsey walisafiri masafa ya mbali kutafuta namna ya kukabiliana na tatizo la njaa ambalo lilikumba kijiji chao. Tunasimuliwa kuwa wanakutana na bibi kizee ambaye aliwasaidia kwa kuwapa dawa ambayo

ingewapatia kila walichohitaji. Hata hivyo, Etsey hakufanikiwa na dawa yake kwa sababu ya tamaa na wivu. Baada ya muhutasari wa ngano teule, tupate muhutasari wa riwaya ya *Kufikirika*.

## 4.0 Muhtasari wa Riwaya ya *Kufikirika*

Katika riwaya ya *Kufikirika,* mwandishi ameichora nchi ya Kufikirika, kaiwekea mipaka yake na kuipa majina yanayosawiri matendo yanayofanywa na wahusika wa nchi hizo. Anaitaja mipaka hiyo kuwa ni nchi ya Anasa kwa upande wa Kaskazini, nchi ya Majaribu kwa upande wa Kusini, Bahari ya Kufaulu iliyoko upande wa Mashariki ikipakana na Safu za Milima ya Jitihada kwa upande wa Magharibi. Mwandishi ameipanga kazi yake katika sura tano ambapo sura ya mwisho ameigawa katika sehemu mbili ambazo ni Baraza na Gereza.

Mwandishi anamwonesha mfalme[1] wa Kufikirika ambaye ni tajiri na mwenye milki kubwa kuliko wafalme wengine. Pia, ni mfalme ambaye amefanikiwa kuwa na kila kitu cha thamani katika nchi yake lakini hakujaliwa kupata mtoto atakayemrithi baada ya utawala wake. Aidha, mfalme anaelewa kuwa licha ya kuwa na mafanikio hayo yote, bado siyo shujaa kama hatakuwa na mtu wa kumrithi baada ya kufa kwake. Hivyo, anaamua kuitisha mkutano wa waganga wote waliopo Kufikirika ili kutafuta tiba ya ugumba wake na wa mkewe.

Mwandishi anaendelea kuonesha kuwa, katika mkutano huo ndipo panapozuka harakati za kuwasaka waganga wa jadi wanaogawanyika katika makundi sita yenye tiba tofauti. Makundi hayo ni kundi la waganga wa mizizi, waganga wa makafara, waganga wa mazinguo, waganga wa hirizi, waganga wa mashetani, na waganga wa utabiri. Makundi matano yanamtibu mfalme pasipo mafanikio na kusababisha nchi kuingia kwenye maafa kutokana na kuchimba mizizi ya kumtibu mfalme, hivyo miti yote inakauka. Aidha, ndege na wanyama wanatoweka kwa sababu ya wingi wa makafara yanayofanywa na waganga, na nafaka zinaisha kwa mazinguo. Mwisho, waganga wa utabiri wanafanikiwa kumtabiria mfalme kuwa atapata mtoto wa kiume ambaye hata hivyo, inatabiriwa kuwa atakapofikisha umri wa miaka kumi atapata maradhi. Ili kuyanusuru maisha yake kutoka katika maradhi hayo atahitaji kufanyiwa kafara la binadamu wawili, mmoja mjinga na mwingine mwerevu.

Mwandishi anaonesha jinsi nchi ya Kufikirika ilivyoingia katika balaa la njaa, maradhi, na vifo kwa kuwa katika kipindi cha miaka sita, Wafikirika hawakuwa wamezalisha chochote zaidi ya kutafuta tiba ya mfalme wao. Mfalme alikuwa anatafuta tiba ya ugumba wake. Hata hivyo, inaoneshwa kuwa kwa kuwa walikuwa na bidii ya kazi, Wafikirika wanafanikiwa kuistawisha tena nchi yao.

[1] Katika uchambuzi wetu, mfalme wa nchi ya Kufikirika ni shujaa.

Mwandishi anaonesha kuwa baada ya miezi tisa tangu utabiri ulipotolewa, mfalme anafanikiwa kupata mtoto wa kiume kama ilivyotabiriwa. Kundi la waganga watabiri linapata heshima kubwa, ambapo kila mganga anapata ijara mara mbili lakini mkuu wa kundi lao anapata ijara mara nne yao pamoja na taji na kutunukiwa jina la heshima, Utubusara Ujingahasara. Historia ya mfalme kupata mtoto inaingizwa pia katika masimulizi na maandiko tangu tiba hadi kupata mtoto.

Mwandishi anatuelezea mambo yaliyotokea baada ya mtoto wa mfalme kufikisha umri wa miaka saba. Tunaoneshwa juhudi aliyoifanya mfalme ya kumtafutia mwanawe mwalimu maalumu na harakati za mwalimu huyu kumfundisha kwa miaka miwili. Tunasimuliwa pia jinsi mwalimu huyu alivyoshindwa kuendelea na kazi kwa kosa la kumfundisha mtoto wa mfalme elimu ya kigeni badala ya ile ya kijadi na historia ya nchi ile. Mwalimu anaacha kazi kwa kuwa hawezi kufundisha elimu ya jadi inayohusiana na makafara ya damu. Tunaelezwa pia jinsi Mfalme alivyoajiri mwalimu mwingine ambaye anampa mtoto maarifa yanayomzidi kiwango kwa muda wa mwaka mmoja. Maarifa hayo yanamsababishia ugonjwa uliomfanya kulala kitandani kwa muda mrefu. Halikadhalika, mwandishi anaendelea kuelezea hali ya afya ya mtoto wa mfalme jinsi ilivyoendelea kuwa mbaya kila alivyokuwa akitibiwa na waganga wa jadi. Mwandishi anaturejesha katika kafara la damu lililokuwa limetabiriwa awali. Mfalme anaomba ushauri wa kafara la damu kwa Waziri Mkuu ambaye pia anaitisha baraza la kuishauri serikali ya Kufikirika juu ya kupitisha sheria ya kafara la damu ya mwanadamu.

Katika riwaya ya *Kufikirika*, mwandishi anawasilisha ujumbe wake huku akionesha sifa mbalimbali za ushujaa na jinsi zinavyosawiri utamaduni na falsafa za Kiafrika. Aidha, ushujaa huu unasawiriwa katika msako wa mtoto, na safari ya msako wa kujitetea na kujinasua kwa mjinga na mwerevu kutoka katika kifo. Hata hivyo, hii siyo safari dhahiri ya kutoka sehemu moja kwenda nyingine kama ilivyozoeleka, bali ya kutoka hali moja kwenda nyingine. Mambo haya yalikuwa muhimu katika makala yetu huku tukiangalia ushujaa katika motifu ya safari ya msako kama inavyosawiriwa na Shaaban Robert katika riwaya ya *Kufikirika*.

## 5.0 Dhana ya Utamaduni na Falsafa ya Kiafrika

Dhana ya utamaduni imeshughulikiwa na wataalamu mbalimbali duniani katika vipindi tofautitofauti vya kihistoria. Kutokana na hilo, kumekuwa na fasili nyingi za dhana hii. Kroeber na Kluckhohn (1952) walikusanya fasili 160 za dhana hii ya utamaduni kutoka kwa wataalamu mbalimbali. Nyerere (1967) akionekana kukubaliana na fasili ya Taylor (1984) anaeleza kwamba utamaduni ndio utambulisho wa taifa lolote duniani. Anasema kwamba nchi ambayo haina utamaduni wake yenyewe ni sawa na mkusanyiko wa watu wasio na 'roho' ya

kuwawezesha kujiita taifa. Hivyo, dhana ya utamaduni inapotumika hapa inarejelea mfumo wa maisha katika jamii fulani. Hii inajumuisha mavazi, lugha, sanaa za maonesho, imani, mila, desturi na kadhalika. Vipengele hivi vinavyounda utamaduni ni vitu vinavyoonekana wazi katika mfumo wa maisha ya mwanadamu ya kila siku.

Kama ilivyo dhana ya utamaduni, dhana ya falsafa ya Kiafrika pia imepata fasili mbalimbali kutoka kwa wataalamu tofautitofauti. Katika miaka ya awali ya uchambuzi wa dhana hii, ilidaiwa kuwa Waafrika hawana falsafa yao, kama anavyosema Maurier (1970:67) kuwa "falsafa ya Kiafrika haipo." Anaeleza zaidi kuwa ingawa tunao watu waliodai kuandika kuhusu kuwapo kwa falsafa ya Kiafrika, kama vile Placide Tempels katika kazi yake ya *Bantu Philosophy* (Falsafa ya Kibantu) na Alexis Kagame katika kazi yake ya *La Philosophie Bantu-Rwandaise de L'Etre* (Falsafa ya Wabantu wa Kinyarwanda), bado dhana hiyo haipo katika jamii za Kiafrika. Anasisitiza kuwa kuna makala na tasnifu nyingi ambazo hazioneshi kuwapo kwa falsafa ya Kiafrika.

Naye Onyeowuenyi (1995:29) anaonesha jinsi wasomi katika vyuo mbalimbali wanavyodharau kuwapo na umuhimu wa falsafa ya Kiafrika. Anasema:

> Ukiangalia katalogi za vyuo vikuu maarufu huko Marekani na Ulaya, utagundua kuwa hakuna idara yoyote ya falsafa inayotoa kozi ya Falsafa ya Kiafrika...vyuo vingi vina vituo vya masomo ya Kiafrika vinavyotoa kozi kuhusu historia ya Kiafrika, sosholojia, fasihi [...] na kadhalika. Lakini hakuna chuo chochote kinachotoa kozi yoyote kuhusu falsafa ya Kiafrika. Idara kubwa za falsafa zinatoa kozi kuhusu falsafa ya Kiasia na Kihindi, lakini kozi ya falsafa ya Kiafrika haipo katika orodha ya kozi zao. Hata nchi changa kama Marekani, nchi inayotambulika mara nyingi kama ya Kimagharibi, sasa ina tawi lake la falsafa (Tafsiri Yetu).

Akitoa mawazo yake kuhusu asili ya falsafa ya Kiyunani, Hegel anasema kuwa asili ya falsafa ya Kiyunani ni Afrika na kwamba Wayunani wamepata misingi ya dini na utamaduni wao kutoka Asia, Syria na Misri (Hegel, 1968:53). Naye Chuachua (2016) akichangia katika mjadala huo, anaeleza kwamba hoja ya Hegel inaonesha kuwa kuna wakati baadhi ya wasomi wa Magharibi wanashindwa kuendelea na msimamo wao wa kuona kuwa Waafrika hawana uwezo wa kufikiri, na kwamba mawazo ya kifalsafa hayawezi kuanzia Afrika. Kuna wataalamu wengine (kama vile Kagame, 1956; Tempels, 1969; Mbiti, 2011) waliofanya tafiti kubainisha kuwapo kwa falsafa ya Kiafrika hasa kwa kujikita kwenye busara ya wazee wakiwa na hoja kuwa suala la elimu rasmi ya shule siyo muhimu tunapobaini falsafa ya Kiafrika. Chuachua (*khj*) anasema kwa kuwa falsafa ni zao muhimu la urazini wa

binadamu, kujenga dhana kuwa Waafrika hawana falsafa ni kuondoa ubinadamu wao.

Kwa ujumla, makala hii inaungana na kazi nyingi za miaka ya karibuni zinazobainisha wazi kuwa, falsafa ya Kiafrika ipo. Hatuwezi kuwa na jamii bila kuwa na falsafa yake kwa sababu ili jamii iwepo, ni lazima iwe na falsafa. Jamii yoyote ni lazima iwe na imani na itikadi zake zinazofafanua kuwapo kwake. Hivyo, jamii za Kiafrika zina imani zake ambazo tunazizungumzia katika makala hii. Imani hizo ndizo falsafa zao (taz. Samwel, 2015; Mulokozi, 2017). Aidha, ieleweke kuwa falsafa na utamaduni ni vipengele pacha ambavyo vinaendana na kuathiriana. Kimsingi, tunapozungumzia falsafa ya Kiafrika, tunazungumzia utamaduni wa Kiafrika. Hata hivyo, haimaanishi kuwa masuala yote ya kifalsafa lazima yawe ya kitamaduni wala masuala yote ya kitamaduni lazima yawe ya kifalsafa. Kwa hiyo, katika kipengele hiki tunapozungumzia utamaduni na falsafa ya Kiafrika inayobebwa na ushujaa unaosawiriwa na motifu ya safari ya msako katika kazi teule, tunazungumzia imani mbalimbali na mienendo ya jamii za Kiafrika inayobebwa na kazi teule.

## 6.0 Ushujaa katika Motifu ya Safari ya Msako na Utamaduni na Falsafa ya Kiafrika

Makala hii imebaini kuwa kuna vipengele mbalimbali vya utamaduni na falsafa ya Kiafrika vinavyobebwa na ushujaa unaosawiriwa katika motifu ya safari ya msako katika ngano za Kiewe na riwaya ya *Kufikirika* ya Shaaban Robert. Vipengele hivyo ni uzazi, umoja na mshikamano, uchawi na uganga au sihiri na imani katika kifo na roho (maisha baada ya kifo). Katika sehemu hii, tumefafanua tamaduni na falsafa hizo kama zinavyojitokeza katika jamii na kazi teule za fasihi.

## 6.1 Utamaduni na Falsafa kuhusu Uzazi

Katika ngano za Kiewe na riwaya teule ya Shaaban Robert utamaduni na falsafa kuhusu suala la uzazi limejibainisha tangu kuzaliwa kwa shujaa kupitia vipengele mbalimbali vya utamaduni na falsafa ya Kiafrika vinavyosawiriwa. Moja ya vipengele hivyo ni suala la kuthamini uzazi kama mhimili wa uendelevu wa jamii inayohusika. Kama tulivyodokeza awali, jamii za Kiafrika huthamini sana uzazi (taz. Igbineweke, 1987; Magesa, 1998; Bujo, 1999; kwa kuwataja baadhi). Kwa mfano, Magesa (1998) anaeleza kwamba ndoa hufungwa kwa lengo moja tu la uzazi. Thamani ya wanandoa katika jamii za Kiafrika hutokana na wanandoa hao kupata mtoto na kinyume chake wanakuwa na thamani ndogo. Igbineweke (1987) na Bujo (1999) wanaeleza kuwa katika jamii za Kiafrika watoto ndio hudumisha jina la ukoo, na ndio hurithi mali za wazee wao. Wanaendelea kueleza kwamba watoto ndio huwa na jukumu la kuwalinda na kuwatunza wazazi wao kipindi cha

uzee wao. Mbiti (1969) anadai kuwa baadhi ya jamii za Kiafrika zenye asili ya Kibantu zinaamini kuwa raha ya ndoa ni watoto na utambulisho wa ndoa yenyewe ni pale tu mwanamke atakaposhika mimba na kuzaa. Katika jamii za Wabantu, hata kama mwanamke atakuwa na sifa nyingine nzuri ambazo zinathaminiwa na jamii yake ikiwa hakubahatika kupata mtoto, basi thamani yake huwa ndogo. Pia, nyumba isiyo na mtoto hujawa na huzuni na huonekana imelaaniwa na wahenga kutokana na kosa kubwa sana lililotendwa. Mbiti (1969) anaendelea kusema kuwa jamii mbalimbali za Kiafrika huwa na harakati za kulitafutia ufumbuzi suala hili la uzazi iwapo kutakuwa na tatizo. Hivyo, kuthamini uzazi ni suala la kiutamaduni na kifalsafa katika jamii za Kiafrika.

Utamaduni na falsafa ya Kiafrika ya kuthamini uzazi inabainika katika ngano za Kiewe na riwaya teule ya Shaaban Robert. Kwa kuanza na ngano za Kiewe, tunaona tamaduni mbalimbali na falsafa hiyo inavyojitokeza. Kwa mfano, katika ngano iitwayo "Baada ya Dhiki Faraja", tunaona furaha ya ndoa ya Kuwornu na mke wake Agbesinyale inavyopotea kutokana na kukosa mtoto. Kutokana na hilo, wahusika hawa mashujaa wanasafiri sehemu mbalimbali kusaka mtoto. Ushujaa unaosawiriwa katika motifu hii ya safari ya msako unabainisha wazi suala la umuhimu wa kuwa na mtoto katika jamii za Kiafrika. Ngano nyingine ni "Mpewa Hapokonyeki." Katika ngano hiyo pia tunaona jinsi mfalme, ambaye ni shujaa anayejengwa na motifu ya safari ya msako, anavyosawiriwa akisaka mtoto kutokana na jamii yake kuthamini mtoto. Kukosa mtoto kulimfanya aonekane kutokuwa kamili na, hivyo, kuibua haja ya kuwa na mtoto.

Zaidi ya kubainika katika ngano za Kiewe na jamii yao kwa ujumla, utamaduni na falsafa ya Kiafrika ya kuthamini uzazi imebainika pia katika riwaya teule ya Shaaban Robert. Hii ni kupitia mhusika mfalme, ambaye ni shujaa, anavyosababisha wahusika mbalimbali na hasa waganga katika riwaya hii kusafiri kuja kumsaidia mfalme kusaka mtoto. Mhusika mfalme, katika riwaya hii, zaidi ya vyote alivyonavyo, alijiona na kuonekana si kitu kutokana na kukosa mtoto. Suala hili linathibitika katika nukuu ifuatayo:

> Nimejaliwa kupata ufalme mkubwa kuliko wafalme wengine walio majirani zangu. Binafsi yangu nimepigana vita vingi kulinda nchi isitekwe na adui… Milki yangu pana imeenea Kaskazini, Kusini, Mashariki na Magharibi. Nimesafiri kuzuru nchi yote iliyo chini ya bendera yangu…nina mali katika hazina inayoweza kununua kitu chochote kinachopatikana kwa thamani kubwa…malkia wangu ni bibi mmoja wa mabibi walio bora na wazuri kabisa katika dunia…nina majeshi ya askari walio shujaa, viongozi hodari na raia wema na watii ambao hawalingani na taifa lolote jingine…lakini nina sikitiko kubwa kwa kukosa mtoto. Maskini mwenye mtoto namwona kuwa ni bora kuliko mimi na pengine moyo wangu huona wivu juu yake (*Kufikirika*: uk. 1-3).

Aidha, suala la uzazi kuwa ni muhimu kuendeleza ukoo na mamlaka linabainika katika riwaya hii ya *Kufikirika* ambapo tunaona mfalme anasema: "Yaonekana kama kwamba matumaini yangu yote ya kurithiwa na mwanangu karibu yatapondwa chini. Mwanangu akipatwa na faradhi msiba utanipeleka ahera mara moja" (*Kufikirika*: uk. 32).

Hivyo, maelezo haya yanaonesha kuwa uzazi unaendeleza ukoo katika jamii za Kiafrika. Jina la mtu linaendelea kupitia mtoto anayezaliwa katika ukoo huo. Kwa hiyo, jina halifi bali linaendelea kupitia mtoto anayezaliwa. Mtoto huyu anapotajwa basi na jina la baba yake linakuwa limetajwa.

**6.2 Utamaduni na Falsafa kuhusu Umoja na Mshikamano**

Umoja na mshikamano kwa jamii nyingi za Kiafrika ni dhana inayojitokeza katika maisha ya kila siku ya Waafrika. Katika jamii za Kiafrika mambo mengi hufanywa kwa kushirikiana baina ya wanajamii na sio mtu peke yake. Watu hushirikiana katika kilimo, malezi ya watoto na maisha kwa ujumla. Huishi kijamaa au kifamilia na mtu anayejitenga akifikwa na tatizo watu humgomea kumsaidia ili aone umuhimu wa kushirikiana. Hivyo, Waafrika wanaamini ushirikiano wa wanajamii ndio huleta mafanikio na kujitenga kwa wanajamii kunasababisha matatizo.

Katika muktadha wa safari ya msako ya shujaa, umoja na mshikamano unajitokeza katika safari ya shujaa pale anapopata msaada wa watu wa jamii yake kama vile msaada wa bibi kizee. Watu wa jamii yake wanamuunga mkono kwa jambo analotaka kulifanya kwa manufaa ya jamii nzima. Kama jamii itakumbwa na mabaa shujaa atajitolea kwa hali na mali ili kuiokoa jamii yake na akifanikiwa huiokoa.

Ngano za Kiewe zimelisawiri suala hili kwa kumchora shujaa ambaye ana ushirikiano na jamii yake kwa kila mambo mema. Kwa mfano, katika ngano iitwayo "Umoja ni Nguvu", mashujaa wanatoka na kusafiri kwa ajili ya kuokoa maisha yao. Kupitia umoja na mshikamano wa farasi, jogoo, paka na mbwa wanafanikiwa kuokoa maisha yao na kuishi maisha ya raha. Vilevile, katika ngano ya "Ujasiri wa Mmoja Huokoa Taifa", Kuchakuro anaenda kuweka mkutano na wanyama wengine na wakapata mawazo ya kumteketeza buibui aliyekuwa akiwaua wanyama wengine ili apate chakula kutokana na balaa la njaa lililoikumba nchi yao. Wanyama walionesha mshikamano na umoja wa kimawazo na wakafanikiwa kumuua adui na kuwanusuru wanyama wengine.

Riwaya ya *Kufikirika* nayo imelieleza jambo hili la umoja na mshikamano kwa kumtumia shujaa mfalme. Mfalme baada ya kutangaza tatizo lake la ugumba, raia wake wote walijitolea hasa wale waliokuwa wana ujuzi wa uganga wa aina tofautitofauti na wakatumia elimu zao kumtibu mfalme hadi akapata ufumbuzi wa

tatizo lake. Umoja na mshikamano huo ulimsaidia mfalme kupata mtoto. Hata mtoto anapoumwa na kukaribia kufa, tunaoneshwa namna jamii nzima inavyoungana pamoja kutafuta njia ya kumtibu mtoto wa mfalme. Mjinga kwa upande mwingine, anaungana na watu wanaokataa kafara ya damu ya mtu ili kumponya mtoto wa mfalme na badala yake, alitafuta njia sahihi ya kumponya mtoto wa mfalme na hivyo kumwokoa mwerevu na jamii nzima ya Kufikirika.

### 6.3 Utamaduni na Falsafa kuhusu Uchawi, Uganga na Sihiri

Utamaduni na falsafa nyingine ya Kiafrika inayosawiriwa na ushujaa unaobebwa na motifu ya safari ya msako unahusu suala la uchawi, uganga na sihiri. Masuala hayo kama tulivyobainisha awali yanaonekana kuwa sehemu ya utamaduni wa jamii za Kiafrika. Ili kuwa katika nafasi nzuri ya kufafanua tamaduni na falsafa kuhusu masuala haya na kuweza kubainisha jinsi yanavyosawiriwa na ushujaa ubebwao na motifu ya safari ya msako katika kazi teule, ni muhimu kuzifafanua kwanza dhana zenyewe kama ifuatavyo:

#### 6.3.1 Utamaduni na Falsafa kuhusu Uchawi

Wataalamu mbalimbali wana mawazo tofautitofauti kuhusu uchawi na masuala mengine kama uganga au ushirikina pamoja na sihiri. Wakati wengine wanaona hakuna utofauti baina ya uganga na uchawi, wengine wanaona masuala hayo ni tofauti kabisa (Evans-Pritchard, 1937; Nukunya, 1992:59). Kwa mfano, Nukunya (1992:59) anasema:

> Mchawi hafanyi tambiko lolote wala hatoi kafara au kusema tabano. Hii itatofautisha wachawi na waganga ambao mara nyingi kazi zao zinahusishwa na matumizi ya vitu halisi ili kupata nguvu za kiungu [...] Nchini Ghana, wachawi wanasemekana kuwa na mikutano ya usiku ambapo maamuzi yanafanyika kuhusu wahanga wao na tendo lenyewe la kuharibu maisha ya watu wengine linafanyika (Tafsiri yetu).

Naye Mbunwe-Samba (1989) anaeleza matendo ya wachawi kuwa ni kuwachukua wahanga ili kuwaua na kuuharibu mwili wao, uhudhuriaji wa mikutano ya usiku. Wazo la Mbunwe-Samba linaendana na la Hamminga (2005:67) anayesema: “Nimeambiwa kuwa mlozi akitumia ungo anaweza kusafiri kwa dakika kumi kutoka Tanzania hadi New York huko Marekani (anasafiri bila mzigo wala kuvaa nguo). Mafuta yake ni damu ya mtu. Unalipa nauli zaidi ya unavyolipa ukisafiri kwa ndege za kawaida.”

Katika makala hii, tunakubaliana na mawazo ya wale wanaosema kuna utofauti baina ya uchawi na uganga, kwa sababu masuala haya yamesawiriwa tofauti na fanani wa ngano za Kiewe na riwaya teule ya Shaaban Robert. Hata

hivyo, mawazo ya wataalamu kuwa upo uwezekano wa mganga kuwa mchawi hayapuuzwi kabisa kwani ni masuala yanayodhihirika katika jamii tulizozitafiti na kazi teule pia. Zaidi ya hilo, mkabala wetu utakuwa ni wa kuzitofautisha kwani hata pale mganga anapoacha kazi yake ya kuganga na kuanza kuharibu, anakuwa si mganga tena bali mharibifu na anastahili kuitwa mchawi.

Kwa mujibu wa Evans-Pritchard (1937), mchawi haharibu ovyoovyo tu. Ili aweze kumroga mtu, anayerogwa anapaswa kuwa mtu wa karibu sana na mchawi huyo. Uhusiano uliotajwa hapa unaweza kuwa wa kifamilia, jirani, rafiki wa karibu, mfanyakazi au mwanafunzi mwenziwe. Uchawi unaweza kurithishwa, kununuliwa au kutafutwa na mtu mwenyewe kwa njia mbalimbali. Akithibitisha hili, Nukunya (1992) anasema kuwa urithi wa uchawi haupo kwa upande wa baba katika ukoo bali unarithishwa na kupokelewa kupitia ukoo wa mama.

Katika ngano za Kiewe, suala la uchawi limesawiriwa kupitia ushujaa unaobebwa na motifu ya safari ya msako. Kwa mfano, tunaona kuwa katika safari ya msako shujaa anasafiri kusaka vitu fulani na vikwazo anavyokutana navyo hutokana na uchawi. Aidha, hata vikwazo vya kawaida katika maisha ya shujaa vinaonekana kunasibishwa na uchawi. Kwa mfano, katika ngano ya "Paka na Panya sio Marafiki", tunamwona fanani akisawiri shujaa anayemlaumu mwenziwe kuwa chanzo cha ugumba wake. Halikadhalika, katika ngano za "Ujasiri wa Mmoja Huokoa Taifa" na "Mkono wa Birika Haufai", tunaoneshwa jinsi uchawi unavyotumika kuharibu na kuua watu wengine. Hadithi hizi zinatuonesha kuwa katika jamii za Waewe, ili uchawi uweze kuwa na madhara kwa anayerogwa, basi mchawi anapaswa kuwa mtu wa karibu sana na yule anayerogwa, kama vile rafiki au jamaa.

Katika riwaya ya *Kufikirika*, mwandishi anatusimulia kuhusu uchawi wa kutumia damu ya mtu kama kafara ili kuokoa maisha ya mtoto wa mfalme. Suala la uchawi linalosawiriwa na kazi teule ni la kitamaduni linalofungamana na falsafa ya Kiafrika. Hata hivyo, katika jamii nyingi za Kiafrika, uchawi ni suala linaloonekana kupigwa vita. Hali kama hiyo pia imebainika katika riwaya ya *Kufikirika* pale ambapo mwandishi anasema:

> Mwalimu ambaye wakati ule wote alikuwa akisikiliza kwa makini mfuriko wa maneno ya mfalme, sasa alitoa jibu. Umefanya vema, Mfalme Mtukufu, kwa kutangulia kunitoa kazi. Kama usingenitoa siku hizi, ningeomba utukufu wako kuamriwa kuacha kazi yako kwa sababu sitaki kushiriki katika makafara ya damu…Damu ina harufu mbaya sana ikimwagwa pasipo sababu ya kutosha. Bora mtu kujitenga kando kabla ya kumwaga damu kuliko kujaribu kujiosha baada ya kumtapakaa (uk. 24).

Nukuu hii inatuonesha kuwa Waafrika wanaamini kwamba uchawi unapaswa kupigwa vita kwani huambatana na uharibifu na ni kikwazo cha maendeleo kama kilivyokuwa kikwazo kimojawapo kikubwa kwa shujaa. Akithibitisha kuwapo kwa utamaduni wa uchawi katika bara la Afrika na ubaya unaoambatana nao, Idowu (1973:9) anasema: "Ninakiri kwa uhakika kuwa, kuna wachawi barani Afrika; hawa wanadhihirika kama wadhihirikavyo wauaji na makundi mengine ya watu waovu…hali hii ambayo ni dhahiri ndiyo msingi wa imani thabiti kuhusu uchawi." Dai la Idowu linathibitisha madai na maoni ya wataalamu wengine kuhusu kuwapo kwa uchawi miongoni mwa Waafrika.

### 6.3.2 Utamaduni na Falsafa kuhusu Uganga na Sihiri

Makala hii imebaini kuwa ushujaa unaosawiriwa katika motifu ya safari ya msako katika kazi teule za fasihi tulizozitafiti umebeba pia utamaduni na falsafa ya Kiafrika kuhusiana na uganga na sihiri. Hili hasa linabainika kupitia ruwaza ya shujaa kupitia vikwazo na majaribu. Baadhi ya mashujaa wanapokumbana na vikwazo au majaribu katika safari zao, hutumia uganga au sihiri kushinda. Katika jamii za Kiafrika, uganga na sihiri huonekana kama njia ya kuondoa tatizo lililopo. Uganga na sihiri huweza kuhusisha matumizi ya dawa za mitishamba, ufanyaji wa makafara, mazinguo, matambiko, maombi kwa mizimu na kadhalika. Matatizo kama vile baa la njaa, ukame, mlipuko wa maradhi kwa binadamu, mifugo au mimea na kukosa mtoto huonekana kuweza kupatiwa ufumbuzi kwa kutumia uganga na sihiri. Utamaduni na falsafa hii ya Kiafrika vimesawiriwa sana katika fasihi ya Kiafrika. Ohly (1981:38) anathibitisha matumizi ya uganga katika riwaya anaposema:

> Katika riwaya, mganga hutimiza majukumu makuu yafuatayo: Huganga ugonjwa wa kimwili, hugundua chanzo cha ugonjwa na mikosi, yaani uchawi na humsaidia mgonjwa kushinda (Tafsiri yetu).

Katika ngano za Kiewe imedhihirika kwamba utamaduni na falsafa kuhusu uganga na sihiri umesawiriwa. Uganga kama ufumbuzi wa matatizo mbalimbali yanayojumuisha baa la njaa na kifo katika jamii, umesawiriwa (taz. Ngano iitwayo "Pacha na Bibi Kizee" na "Wivu Haufai"). Katika ngano hizi, fanani anaonesha namna mashujaa walivyokumbana na matatizo mbalimbali kama vile njaa. Vikwazo hivi vilihitaji shujaa kutumia njia ya uganga ili aweze kupata chakula kusaidia jamii. Aidha, katika ngano za Kiewe, tunaona inasawiriwa kwamba mchawi huweza kusababisha tatizo na mganga huweza kulitatua. Kwa mfano, katika ngano iitwayo "Paka na Panya sio Marafiki", paka anaamini kuwa tatizo lake la ugumba limesababishwa na kitu kibaya (uchawi) alichofanyiwa na panya. Kutokana na hilo, paka anakubali kupelekwa sehemu (kwa mganga) ili apatiwe ufumbuzi wa tatizo

lake. Si hivyo tu, bali pia suala la uganga linasawiriwa katika motifu ya safari ya msako inayotumiwa katika ngano zifuatazo za Kiewe: "Usisahu Asili Yako", "Asana na Fuseini" na "Asiyesikia la Mkuu Huvunjika Guu". Katika ngano hizo, tunaelezwa jinsi uganga na sihiri vilivyosaidia kutatua tatizo la kutopata watoto. Tatizo hilo liliwasumbua sana mashujaa wa ngano husika kiasi cha kusafiri huku na huko wakisaka mtoto. Katika safari hizo za msako wanakwenda kwa waganga ambao wanawapatia ufumbuzi wa ugumba na wao kuwa mashujaa. Kwa mfano, katika ngano iitwayo "Usisahu Asili Yako", fanani analithibitisha hili anaposema:

> Hapo zamani za kale, kulikuwapo mwanamke tasa mmoja. Alikuwa anachekwa sana na marafiki zake pale kijijini kwa kuwa hana mtoto. Alitafuta matibabu sehemu nyingi, kwa waganga, alikunywa kila aina ya dawa ili kupata mimba, lakini hakufanikiwa.

Kwa upande wa ngano iitwayo "Asana na Fuseini", tunaona shujaa anapokutana na vikwazo mbalimbali, anatumia nguvu za uganga na sihiri ili kuvishinda. Katika ngano hii, ilipotokea Fuseini amechukuliwa na Chunusi, shujaa Asana anasafiri kwenda kumsaka. Ili kufanikiwa, Asana anatumia nguvu ya uganga na sihiri aliyopewa na wazazi wake kupambana na Chunusi. Rejea fanani wa hadithi hii anaposema:

> Alizamia chini zaidi ingawa alipata shida kupumua, aliamua kutumia nguvu alizopewa na wazazi wake ili aishi chini ya maji bila shida yoyote huku akimtafuta kaka yake. Baada ya kutembea kwa masiku chini ya maji bila hata chakula, siku moja, alimkuta Chunusi amelala. Asana alikwenda na kupambana naye mpaka akamzidi nguvu Chunusi na kumuua, kisha akamuokoa kaka yake akiwa bado hai. Walirudi kutoka kwenye maji na wakaishi kwa furaha.

Mbali na uganga kusawiriwa na ngano za Kiewe kutoka Ghana, uganga pia unaonekana kuwa mojawapo ya masuala ya kitamaduni katika jamii za Kitanzania. Hili linathibitishwa na Chuachua (2016: 241) anayesema, "Utafiti wa uwandani umethibitisha kuwa Chifu Mkwawa alikuwa mganga na mtabiri. Kwa uganga wake alitabiri kwa usahihi mwelekeo wa adui." Suala la utamaduni na falsafa ya uchawi katika jamii za Kitanzania, na Afrika Mashariki kwa ujumla, linazungumzwa pia na Sengo (1992:49) anaposema:

> Itikadi za Waswahili wa mwambao wa Kenya ni pamoja na imani ya kuwapo pepo-majini, mashetani na kadhalika nguvu na uwepo wa pepo hao katika kulinda mashamba, mali, miji, kusaidia kutibu maradhi, na mashetani kuroga na kadhalika. Itikadi hizi zina nafasi katika upwa wote wa Waswahili. Pamoja nazo, Waswahili wana mila kama vile ya miiko mbalimbali. Mifano: kula gizani ni kula na shetani. Kunywa maji msalani

> mtu huwa mwongo. Bundi akilia juu ya nyumba anatangaza kifo na kadhalika. Mbaabu anamalizia sura hii ya mwisho wa kitabu chake na maneno haya: "Itikadi …zina mafunzo mengi yanayostahili kuhifadhiwa na kuzingatiwa."

Utamaduni na falsafa kuhusu uganga unasawiriwa sana na kazi za fasihi za jamii za Afrika Mashariki. Katika jamii hizo, inabainika kwamba mashujaa walio wengi huonekana kutotegemea nguvu za akili na kimwili pekee kwani zenyewe peke yake hazisaidii. Badala yake wanategemea pia nguvu za kisihiri au kiganga zitakazowasaidia kushinda vikwazo na maadui zake. Kwa mfano, Mulokozi anapozungumzia nguvu aliyonayo Liyongo, mmoja wa mashujaa wa Afrika Mashariki, anasema, Liyongo alikuwa na nguvu ya uganga au sihiri (taz. Mulokozi, 1999:14- I5). Katika riwaya teule tunaona pia utamaduni na falsafa kuhusu uganga umesawiriwa kupitia ushujaa unaobebwa na motifu ya safari ya msako. Kwa mfano, katika riwaya ya *Kufikirika*, Shaaban Robert anatuonesha kuwa uganga ndicho chanzo cha baraka ya kupata watoto na suluhisho la tatizo la ugumba. Hii ni dhahiri kuwa uganga unaosawiriwa hapa ni suala la kitamaduni na kifalsafa katika jamii za Kitanzania. Hivyo, ushujaa unaosawiriwa na motifu ya safari ya msako katika riwaya hii, unabeba utamaduni na falsafa ya Kiafrika kuhusu uganga kama suluhisho la matatizo mbalimbali.

### 6.4 Utamaduni na Falsafa kuhusu Imani katika Roho na Kifo

Mbali na tamaduni na falsafa hizo za Kiafrika zinazosawiriwa na ushujaa katika motifu ya safari ya msako kwenye kazi teule za fasihi, utamaduni na falsafa nyingine ni kuhusu imani katika roho na kifo. Kama ilivyodokezwa awali, jamii za Kiafrika huamini kuwa, mbali na shujaa kuzaliwa na shujaa kukutana na majaribu, shujaa pia huweza kufa. Tumedokeza kuwa Waafrika hawaamini katika kifo, bali hupitia kutoka maisha ya dunia hii kuingia katika maisha ya umilele, kwani roho za watu waliokufa huendelea kuwapo katika dunia hii kupitia majina.

Waafrika huamini zaidi kwamba, mtu anapokufa ndipo mtoto mwingine anapozaliwa. Mbali na imani hiyo, Waafrika pia huamini kwamba kuna uhusiano mkubwa baina ya walio hai na wafu. Tempels akizungumzia uhusiano baina ya watu waliokufa na walio hai katika jamii za Kiafrika anasema kuwa: "Roho za waliokufa hutafuta makao yao katika miili ya walio hai, na kuendelea kuwapo duniani" (Tempels, 1969:22). Naye Chuachua (2016) anazungumzia hili kwa kurejelea utafiti wa Hallen na Sodipo (1997) katika jamii za Wayoruba. Katika utafiti huo, inaelezwa kuwa nafsi ya mtu katika jamii za Wayoruba imegawanyika katika sehemu tatu na kwamba roho (*emi*) huendelea kuwapo baada ya kifo. Akizungumzia imani za Waafrika kuhusu kifo, Mbiti (1995:79-80) anaeleza:

> Kama tutapanga kwa kuzingatia hadhi au madaraja, tunaweza kusema kuwa mizimu ni viumbe wa kawaida wa kiroho walio karibu na daraja la miungu lakini juu ya hadhi ya wanadamu…watu wengi huonekana kuamini kuwa, mizimu ni kile kinachobaki baada ya kifo cha kimwili cha binadamu. Kuwa mzimu ni kama kupandishwa hadhi ya kijamii. Kwa sababu hiyo, Waafrika huwaheshimu wafu-hai wao (Tafsiri yetu).

Aidha, Nukunya (1992), akizungumzia jamii ya Waewe na imani hii, anaonekana kuungana na Mbiti na anasisitiza kuwa, nafasi ya kupandishwa hadhi kwa viumbe wa kiroho imewekwa kwa ajili ya wahenga ambao waliishi maisha mazuri na kuacha mifano mizuri ya kuigwa na jamii, na pia kufariki kwa kifo cha heshima. Nukunya (khj: 56) anaendelea kuzungumzia imani katika kifo miongoni mwa jamii ya Waewe wa Ghana na kusema:

> Kifo sio mwisho wa maisha ya binadamu. Kifo kinapotokea, ni mwili wa binadamu unaoharibika lakini nafsi yake inaenda katika nchi ambapo kuna roho za wafu wengine kujiunga nao. Katika nchi ya roho, wafu wana uwezo wa kutawala mambo ya dunia ya binadamu wakiadhibu wanaovunja sheria na kuwapongeza wale wanaoendana na tabia zinazokubalika (Tafsiri yetu).

Katika utamaduni wa Waewe, kama ilivyo kwa Waafrika wengine, mtu yeyote anayezaliwa ana siku maalum ambapo atakufa. Hata hivyo, kama tulivyofafanua hapo awali, Waewe huamini kwamba mtu hafi bali kifo ni kitendo cha mtu kupitishwa kutoka katika ulimwengu huu na kuingia katika ulimwengu mwingine, ambapo anakutana na wahenga wengine waliotangulia.

Pia, ruwaza ya kifo cha shujaa, kama zilivyo ruwaza nyingine zilizotumika kufafanua ushujaa katika motifu ya safari ya msako, huakisi falsafa za Kiafrika. Hili linabainika katika ngano za Kiewe tulizozishughulikia. Katika ngano ya "Asiyesikia la Mkuu Huvunjika Guu", fanani anatumia kifo cha shujaa kuonesha namna kinavyoakisi utamaduni na falsafa ya Kiafrika kuhusu kifo. Katika jamii hizi kifo si ishara ya kushindwa kwani shujaa anapokufa anapita kutoka katika daraja la walio hai na kwenda katika dunia nyingine ambapo anakuwa na nguvu na uwezo zaidi. Kwenye ngano hii tunaona kuwa shujaa anapokufa anaenda kujiunga na wahenga waliotangulia. Katika ngano za "Paka na Panya Sio Marafiki" na "Ujasiri wa Mmoja Huokoa Taifa", tunabaini jinsi tamaduni na falsafa kuhusu kifo zinavyosawiriwa. Tunaona katika ngano hizo, jinsi mashujaa walivyopambana na maadui katika safari yao ya msako na kuzidiwa jambo lililosababisha vifo vyao. Hata hivyo, wanapokufa wanaoneshwa kuendelea kuishi. Hii ni ithibati kwamba ngano za Kiewe zinasawiri tamaduni na falsafa za Kiafrika.

Kwa upande wa riwaya teule, tumebaini kuwa riwaya ya Shaaban Robert inabeba pia tamaduni na falsafa za Kiafrika kuhusu kifo. Shaaban Robert anaonekana kuamini katika kuwapo kwa kifo na kuwa kifo si mwisho wa kuwapo kwa mwanadamu. Maelezo yote haya yanathibitisha imani ya Waafrika juu ya maisha yao baada ya kifo na kuwa, kifo ni mapito tu katika dunia hii.

## 7.0 Hitimisho

Katika makala hii tumetazama namna ushujaa unavyobainika katika motifu ya safari ya msako na jinsi unavyoakisi utamaduni na falsafa ya Kiafrika. Pia, makala hii kupitia ngano za Kiewe na riwaya ya *Kufikirika* imebainika kwamba Waafrika wana imani tofautitofauti juu ya ulimwengu na mazingira yao. Siku zote wamekuwa wakiishi huku wakiongozwa na imani hizo juu ya ulimwengu wao. Aidha tumetumia ruwaza ya shujaa kwa mujibu wa Campbell ambazo ni kuondoka, kukutana na vikwazo na kuvishinda, na kurudi katika jamii. Makala hii imebaini kuwa kuna vipengele mbalimbali vya utamaduni na falsafa ya Kiafrika vinavyobebwa na ushujaa unaosawiriwa katika motifu ya safari ya msako katika ngano za Kiewe na riwaya ya *Kufikirika*. Kupitia hayo, makala hii imethibitisha kwamba Waafrika huamini katika uzazi, umoja na mshikamano, uchawi na uganga au sihiri na imani katika kifo na roho (maisha baada ya kifo).

## Marejeleo

Brown, L.T. (1990). *The Hero's Journey, Joseph Campbell on His Life and Work.* New York: Harper and Row.

Bujo, B. (1999). *African Theology in its Social Context*. Nairobi: Paulines Publications.

Campbell, J. (1973). *The Hero with a Thousand Faces.* Princeton: Bolingeu.

Chuachua, R. (2016). Falsafa ya Riwaya za Shaaban Robert Robert na Euphrase Kezilahabi katika Muktadha wa Epistemolojia ya Kibantu. Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Dodoma.

Dzakpasu, T.E. (1981). Gli: An Ewe Performance Art. Master of Arts Dissertation (Unpublished). University of Ghana, Legon.

Evans-Pritchard, E.E. (1937). *Witchcraft, Oracles and Magic among the Azande.* Oxford: Clarendon Press.

Hallen, B. and Sodipo, J.O. (1997). *Knowledge, Belief and Witchcraft: Analytic Experiments in African Philosophy.* Palo Alto: Standford University Press.

Hamminga, B. (2005). *Knowledge and Cultures: Comparative Western and African Epistemology*. New York: Rodopi.

Hegel, G.F.W. (1968). *Philosophy of History*. New York: Dover Publications Inc.

Idowu, E.B. (1973). *African Traditional Religion: A Definition.* Lagos: Orbis

Books.
Igbineweke, F.E. (1987). *The Sacrament of Marriage and Childlessness in the Edo Pastoral Problems and Possible Solutions.* Rome: Tipogrfica Leberit.
Kagame, A. (1956). *La Philosophie Bantu-Rwandaise de L'Etre*. Bruxelles: Academie Rayole des Sciences Coloniales.
Kroeber, A.L. and Kluckhohn, C. (1952). *Culture: A Critical Review of Concepts and Definition* New York: Vantage Books.
Kunene, D.P. (1985). "Journey as Metaphor in Africa Literature" Stephen A. Mh. African Literature Studies: The Present State/L' et al., Present. Washington: Three Continents Press.
Magesa, L. (1998*). African Religion*: *The Moral Traditions of Abundant Life*. Maryknoll: Orbis Books.
Maurier, H. (1970). "Do we Have an African Philosophy?" Katika R. A. Write (Ed.). *African Philosophy: An Introduction.* Linham: University Press of America. pp. 67-78.
Mbiti, J.S. (1969). *African Religion and Philosophy.* London: Heinemann.
Mbiti, J.S. (1995). *African Religion and Philosophy*. London: Heinemann.
Mbunwe-Samba, P. (1989). *Witchcraft, Magic and Divination: A Personal Testimony*. Bamenda: Archives Edition.
Mulokozi, M.M. (Mh.) (1999). *Tenzi Tatu za Kale*. Dar es Salaam: TUKI.
Mulokozi, M.M. (2017). *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili*: *Kozi za Fasihi Vyuoni na Vyuo Vikuu*. Dar es Salaam: KAUTTU.
Nukunya, G.K. (1992). *Tradition and Change in Ghana: An Introduction to Sociology.* Accra: Ghana University Press.
Nyamsenda, J.C. (2015). Ushujaa wa Shujaa wa Motifu za Safari na Msako katika Ngano za Waikizu, Wabondei na Wazanzibari. Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa), Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania.
Nyerere, J.K. (1967). *Freedom and Unity, Uhuru na Umoja: A Selection Form Writings and Speeches 1952-65.* Dar es Salaam: Oxford University Press.
Maurier, H. (1970). "Do we Have an African Philosophy?" Katika R. A. Write (Ed.). *African Philosophy: An Introduction.* Linham: University Press of America. pp. 67-78.
Ohly, R. (1981). *Aggressive Prose.* Dar es Salaam: TUKI.
Onyeowuenyi, I. (1995). "Is There an African Philosophy?" Katika *African Philosophy Selected Readings.* New Jersey: Prentice Hall.
Robert, S. (1967). *Kufikirika.* Nairobi: Oxford Universty Press.
Samwel, M. (2015). *Umahiri katika Fasihi.* Dar es Salaam: MEVELI Publishers.
Sengo, T. S. Y. (1992). "Utamaduni wa Kiswahili: Wilaya ya Kusini-Unguja." *Nordic Journal of African Studies.* pp. 53-79.

Senkoro, F.E.M.K. (1997). ‘The Significance of the Journey in Folktales from Zanzibar. Unpublished PhD Thesis. University of Dar es Salaam.
Sungi, N.A. (2011). Ruwaza ya Shujaa Mwanamke wa Kiutendi katika jamii ya Wanyanyembe wa Tabora. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
Tempels, P. (1969). *Bantu Philosophy*. Paris: Presence Africaine.

# KIAMBATISHO
# MFANO WA NGANO YA WAEWE NA TAFSIRI YAKE YA KISWAHILI

| NGANO ZA KIEWE | TAFSIRI YA KISWAHILI |
|---|---|
| ***Asana kple Fuseini***<br>***Glitola:*** *Mise mise gli looo!*<br>***Gliselawo:*** *Gli neva.*<br>***Glisela:*** *Gli tso vuu dze Asana kple Fuseini dzi.*<br>***Gliselawo:*** *Wòdze wo dzi.*<br><br>*Eva dzɔ gbe deka bena, nyɔnuvi ade nɔ anyi si nukɔe nye Asana kple nɔvia nutsuvi si nukɔe nye Fuseni. Asana kple Fuseni nye venɔviwo eye woyina teƒe desiade dekae. Le ƒe gedewo megbe la, wodzilawo ku. Venvvieve siawo kpe fu gede nutɔ elabena ameadeke meli si akpe de wo nu o. Wodze toƒo dede gɔme ne woade nudonui adzra bena watenu akpɔ ga aƒle nududu. Wowɔ dɔ sia ƒe gedewo sɔɔ elabena nuwo nɔ sesem nawo. Gbe deka la esime woyi tɔƒo be yewoava di lã la, kasia lã gã ade si nye aboso la va le Fuseini hekplɔ yi de tɔ la te eye Asana deka tsi anyi gake edui bena yade yenɔvi la. Eyata nukeke adre sɔɔ la, Asana nɔ vɔsasa dzi hele dzila ŋɔliwo yom bena woaxɔ yeƒe gbedododa yina Mawu dzifo vii tɔ bena yatenu akpɔ yenɔvi la agbagbee.*<br><br>*Gbe deka la, Asana dui be yayi tɔ la te adavadi Fuseini. Eyi tɔ la te vii togbɔ bena ekpe fu gede be yeakpɔ gbɔgbɔ, mloeba la edui bena yaza nuse si edzilawo tsɔne bena watenu anɔ tɔ la te fumakpemakpee na woadi nɔvia la. Esime wòtsa le tɔ la me numadumadui la, evake de boso la nu si dɔ alɔ. Asana yi dakpe ava kple boso la vasede esime eƒe nuse kpe boso la dzi eye wòwui, emegbe la, ede nɔvia si tsi agbe. Wo ame eve la do le tɔ la me eye wonɔ anyi kple dzidzɔ*<br>**Glitola***: Esia nye gli sia ƒe nu wuwu. Adze se to gobui mi*<br>**Gliselawo***: Adze du mi wò.* | **Asana na Fuseini**<br>Msimulizi: Sikilizeni sikilizeni hadithi looo!<br>Hadhira: Hadithi Njoo.<br>Msimulizi: Hadithi iliwaangukia Asana na Fuseini.<br>Hadhira: Iliwaangukia.<br>Hapo zamani za kale, aliishi msichana aliyeitwa Asana na kaka yake aliyeitwa Fuseini. Asana na Fuseini walikuwa pacha na walikwenda kila mahali pamoja. Baada ya siku kupita, wazazi wao walifariki. Waliteseka sana kwa sababu hapakuwapo na mtu yeyote wa kuwasaidia. Walianza kuvua samaki ili waweze kuuza na kupata chakula. Waliendelea na kazi hiyo kwa sababu maisha yalikuwa magumu kwao. Siku moja walipokwenda kuvua, kulikuwa na samaki mkubwa, alikuwa ni Chunusi.<br><br>Chunusi alimchukua Fuseni na kumpeleka chini ya maji na Asana aliachwa peke yake na akaamua kumwokoa kaka yake. Kila siku huenda mtoni ili kuona kama atafanikiwa kumuokoa kaka yake. Kwa siku saba mfululizo Asana alikuwa anaomba kwa kuita roho za marehemu wazazi wake na kutoa kafara mbalimbali huku akiziita roho za wazazi wake zimsaidie na kufikisha maombi yake kwa Mwenyezi Mungu ili aweze kumpata kaka yake tena akiwa hai. Siku moja Asana aliamua kuzamia kwenye maji na kumtafuta kaka yake.<br><br>Alizamia chini zaidi ingawa alipata shida kupumua, aliamua kutumia nguvu alizopewa na wazazi wake ili aishi chini ya maji bila shida yoyote huku akimtafuta kaka yake. Baada ya kutembea kwa siku kadhaa chini ya maji bila hata chakula, siku moja, alimkuta Chunusi amelala. Asana alikwenda na kupambana naye mpaka akamzidi Chunusi na kumua, kisha akamuokoa kaka yake akiwa bado hai. Walirudi kutoka kwenye maji na wakaishi kwa furaha.<br>**Msimulizi:** Huu ndio mwisho wa hadithi yangu.<br>**Hadhira:** Kumbe? Basi ulimi wako upakwe mafuta<br>**Msimuliaji:** Na masikio yenu yatiwe mafuta. |